

Mshiriki wa Mafunzo:	Mwezeshaji:	Tarehe:
----------------------	-------------	---------

Mambo Muhimu	Maoni ya Mwezeshaji	Ndio	Hapana
<b>Kabla ya kufanya kipimo cha Uoni</b>			
1. Kuweka vizuri eneo la kufanyia kazi ili liwezekutumika: <ul style="list-style-type: none"> <li>Liwe na mwanga wa kutosha, na lisilopigwa na jua moja kwa moja au lenye moto</li> <li>Kuwepo kiti kwa ajili ya Mteja na yeye Mtoa huduma</li> <li>Kifaa cha kupimia kiwe tayari</li> </ul>			
2. Kutoa maelezo kuhusu Kipimo cha Uoni: <ul style="list-style-type: none"> <li>Ainisha yaliyoko kwenye kipimo cha Uoni.</li> <li>Elezea kuwa sio kipimo hitimisho cha Uoni.</li> <li>Mruhusu mteja kuuliza maswali</li> <li>Muulizie mteja kama anaridhia kufanya kipimo</li> </ul>			
<b>Kipimo rahisi cha Afya ya Macho</b>			
3. Osha macho kabla na baada ya kufanya kipimo			
4. Angalia dalili za macho yenye matatizo: <ul style="list-style-type: none"> <li>Washa tochi kwa usahihi ili kuona jicho</li> <li>Anainisha dalili za jicho lenye matatizo</li> <li>Angalia kama rufaa inahitajika</li> </ul>			
5. Muulize mteja kama ana Ugonjwa wa kisukari na maumivu ya jicho au hali ya kutokujisikia vizuri. <ul style="list-style-type: none"> <li>Angalia kama rufaa inahitajika</li> </ul>			
<b>Kipimo rahisi cha Uoni wa Umbali mrefu</b>			
6. Tumia kwa usahihi chati ya herufi E katika umbali sahihi ili kupima Uoni wa mbali <ul style="list-style-type: none"> <li>Elezea kipimo na muombe mteja kuvaa miwani kama inahitajika,</li> <li>Pima jicho moja baada ya jingine</li> <li>Onyesha herufi sahihi za E katika mtiririko sahihi.</li> </ul>			
<b>Kipimo cha karibu cha Uoni</b>			

<p>7. Anaonyesha kwa usahihi Chati ya herufi E katika umbali sahihi ili kupima uwezo wa Uoni wa karibu</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Elezea na muombe mteja kuvaa miwani pale inahitajika.</li> <li>• Fungua macho</li> <li>• Onyesha herufi za E katika mtiririko sahihi.</li> </ul>			
<b>Anajadili na kukubaliana na mteja kuhusu hatua zinazofuata</b>			
<p>8. Toa tafsiri sahihi ya matokeo ya kipimo na elezea hatua zitakazofuata</p>			
<b>Wakati wote wa kipimo</b>			
<p>9. Katika utekelezaji wa hatua zote, onyesha kuwa huduma unayoitoa ni salama na inayomjali mteja .</p>			

**Mambo ya kuzingatiwa na Mwezeshaji.****Tumia Orodha hii ya stadi kukusaidia:**

- Tathmini namna Washiriki wa Mafunzo wanavyotekeleza stadi za Ufanyaji wa kipimo rahisi cha Uoni na kama:
  - Wanaweza kufanya kipimo rahisi cha Uoni bila kupewa msaada kutoka kwa mtu mwingine, au
  - Wanahitaji mafunzo zaidi ya vitendo na kama ndicho hicho wanachokihitaji, tambua aina ya stadi wanazohitaji kufanyia mazoezi.

**Kumbuka kuwa:**

- Hii Orodha ina Stadi muhimu ambazo ziko kwenye moduli ya TAP.
- Kuna stadi nyingine ambazo ungependa Watoa huduma wako kuwa nazo kulingana na mahitaji ya huduma wanazozitoa. Unaweza kuongeza mambo mengine kwenye Orodha hii kama kwa kufanya hivyo itasaidia zaidi.

**Ili kutumia Orodha ya Stadi:**

- Fuatilia kwa karibu namna ambavyo Washiriki wa Mafunzo wanafanya kipimo rahisi cha Uoni. Hii naweza kufanyika kwa kufanya igizo (mmoja akiwa Mteja mwingine kama Mtoa huduma) au kufanya igizo na Wateja.
- Hakikisha kuwa zoezi na Wateja linafanyika kwa usalama.
- Andika kwenye fomu kama Mshiriki wa Mafunzo amefanya kila stadi kwa usahihi. Andika maelezo kwenye eneo la kutoa maoni. Hii inaweza kuwa vitu ambavyo Mshiriki wa Mafunzo amefanya vizuri Zaidi au maeneo ambayo anapaswa kuboreshwa Zaidi/anahitaji mafunzo Zaidi.

**Utoaji wa mrejesho kwa Washiriki wa Mafunzo**

- Jadili na Washiriki wa Mafunzo kuhusu mambo uliyoyaona. Wajulishe mambo wanayoyafanya vizuri na maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.
- Wape nakala ya Orodha ya Stadi iliyokamilika kwa ajili ya wao kuweka kumbukumbu.
- Endelea kutoa mafunzo kwa vitendo na msaada pale unapohitajika na fanya tathmini mara kwa mara ili kuboresha stadi na kujenga hali ya kujiamini.

**Ni wakati gani Mshiriki wa Mafunzo anaweza kufanya kipimo rahisi cha Uoni bila ya kupata usaidizi?**

- Ili kuafnya kipimo cha Uoni kwa usalama zaidi, mshiriki wa mafunzo anapaswa kukamilisha stadi zote kwa usahihi.
- Kumbuka- kutoa mafunzo kwa vitendo na kusimamia ni mchakato endelevu ili kuboresha stadi.